Uchunguzi wa Masuala ya Kijinsia katika Nyimbo za Daudi Kabaka na John Amutabi Nzenze

Shadrack Opunde, Sheila Wandera, Wendo Nabea
Laikipia University, Kenya

Abstract

Sexuality and gender issues are some of the emerging issues in our society today. The concept of gender has been under discussion by various scholars in different dormains such as social, economic, political and educational spheres. This paper aims at outlining and analysing gender issues as depicted in the songs of Daudi Kabaka and John A. Nzenze famously known as 'zilizopendwa'. Moreover, the paper explores changes in gender issues with time. Daudi Kabaka and John Nzenze are legendary musicians from Luhya community whose songs majorly featured in 1950, 1960 and 1970 commonly known as 'twist'. A song is a short poem or piece of music which combines melody and vocals. Songs belong to one of the genres of oral literature. Songs elaborate some of the issues happening in the society with focus on relationships in the society, different conflicts, irony, soothing, entertainment, streamlining bebaviour, moral and cultural transmission. Ethnographic design and the library method of data collection were used respectively. Ethnographic research design was vital in helping description and collecting qualitative data on different traditions. It was also used to help explore and understand gender issues in Daudi Kabaka and John Nzenze songs because it focused on a particular community. The paper was guided by African feminism theory as propounded by Steady (1981). This paper is significant because it gives a clear picture of a woman in a patriarchal society and ways through which the woman has been using to get her emanicipation.

Keywords: African feminism, gender, songs, twist.

Ikisiri

Masuala ya kiuana na kijinsia ni mojawapo ya masuala ibuka yanayotokea katika jamii za kisasa. Dhana ya kijinsia imekuwa ikijadiliwa na wataalam mbali mbali ambao wamekuwa wakiangazia nyanja tofauti kama vile, kijamii, kiuchumi, kisiasa na kielimu. Makala hii ilinuia kuainisha na kuyachambua masuala ya kijinsia jinsi yalivyojitokeza katika nyimbo za zilizopendwa za Daudi Kabaka na John A. Nzenze. Aidha ilijadili mabadiliko ya masuala ya kijinsia katika jamii. Daudi Kabaka na John Nzenze ni wanamuziki wakongwe kutoka jamii ya Waluhyia walioimba nyimbo za mitindo ya kipekee kwa jina la twist katika miaka ya 1950, 1960 na 1970. Nyimbo ni tungo zenye mahadhi ya sauti ya kupanda na kushuka na ni mojawapo ya vipera vya fasihi simulizi. Nyimbo huzungumzia masuala mazito ya kijamii na hupania kuonyesha uhusiano wa kijamii, migogoro mbalimbali, kukejeli, kuliwaza, kubembeleza, kutumbuiza, kuongoa na kuburudisha na kupitia maadili na utamaduni wa kijamii. Makala hii ilizingatia utafiti maktabani na ukatumia mkabala wa kiethnografia ambao ulinuia kukusanya data za kimaelezo na kina kuhusu tamaduni za jamii mbali mbali. Mkabala huu ulikuwa muhimu katika kuelekeza na kubainisha masuala ya kijinsia yaliyojitokeza katika nyimbo za Daudi Kabaka na John Nzenze kwa kuangazia jamii mahususi. Makala hii iliongozwa na nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika jinsi ilivyoasisiwa na Steady (1981). Aidha makala hii imejadili kwa kuangazia mtazamo wa kijamii kuhusu jinsi masuala ya kijinsia yamekuwa yakibadilika kadri muda unavyobadilika. Makala hii ni muhimu kwa sababu inatuchorea taswira halisi ya mwanamke katika jamii ya ubabedume na kuonyesha njia ambazo amekuwa akizitumia katika kupigania hali hizi pamoja na kupata ukombozi

Maneno muhimu: Nyimbo, uana, ufeministi wa kiafrika, twist.

Utangulizi

Fasihi simulizi ni sanaa ambayo huwasilishwa kupitia kwa njia ya masimulizi katika jamii. Hususan, ni fasihi ambayo huchukuliwa kumaanisha jumla ya tajriba ya maisha ya watu. Tajriba hizo hudhihirika kupitia mawasiliano ya lugha, mifumo ya kijamii kama vile nyimbo za tohara, hisia, imani, ushirikina, tabia na mazoea na ufundi na mbinu wazitumiazo watu kukidhi mahitaji ya kimaisha (Simala, 2006). Fasihi simulizi ni nembo ya jamii na huwasilisha falsafa mbalimbali za jamii husika. Ufafanuzi mbalimbali umetolewa ili kuelezea dhana ya nyimbo. Nyimbo ni kipera cha utanzu wa ushairi simulizi wa fasihi simulizi.

Wataalam mbalimbali wanafafanua dhana ya nyimbo kwa namna zifuatazo. Kwa mfano, Mulokozi (1981) anayeeleza dhana ya wimbo kwa kutolea sifa zake kama vile: muziki wa ala unaotumiwa kuwasilisha maudhui fulani, muziki wa sauti ya mwimbaji ulio na ufundi wa kipekee katika uwasilishaji wake, matini au maneno yanayoimbwa yanayobeba maudhui mbali mbali, hadhira inayoimbiwa na inayohusika na kuchangia kwa njia moja au nyingine na muktadha wa uimbaji kama vile ibaada, sherehe na matanga na kadhalika.

Kamusi ya TUKI (2010) inaeleza dhana ya wimbo kwa kusema kuwa, wimbo ni maneno yanayotamkwa kwa sauti ya muziki. Kwa mujibu wa King'ei na Kisovi (2005), wimbo ni utungo ambao una mpangilio maalum wa maneno na una mahadhi. Nyimbo huweza kuimbwa na mtu mmoja au kikundi na huhusishwa na maneno kuhusu jambo fulani na pia sauti ya mwimbaji au waimbaji. Isitoshe, kwa mujibu wa M'Ngaruthi (2008) wimbo ni maneno yanayotamkwa kwa sauti na kuvutia kwa mahadhi ya kupendeza.

Kutokana na maelezo haya tunaweza kufafanua dhana ya wimbo kwa kusema kuwa, wimbo ni sanaa ya fasihi simulizi ambayo hutumia lugha teule, sauti na kiimbo maalum kwa kutumia ala za muziki kama vile ngoma na nyinginezo katika kuwasilisha maudhui yake yanayohusiana na jamii au muktadha maalum. Maudhui katika nyimbo huhusishwa na muktadha wa jamii. Kwa hivyo, nyimbo huwa kioo cha jamii. Nyimbo zinaweza kuimbwa na mtu mmoja au zaidi na hugawanywa katika beti na mishororo. Nyimbo nyingi huwa na kiitikio au mstari ambao hurudiwarudiwa. Maelezo haya yanaafikiana na dhana nyimbo na hivyo muhimu katika kueleza dhana ya nyimbo katika muktadha wa nyimbo za mtindo wa *twist.*

Nyimbo za mitindo ya *twist* ni nyimbo zinazopatikana katika aina ya zilizopendwa. Nyimbo za zilizopendwa ni zile zilizoimbwa kuanzia miaka ya 1950-1980 na kuendelea wakati nchi za Afrika Mashariki zilikuwa zikipigania ukombozi wake kutoka kwa wakoloni. Ni nyimbo zilizojadili masuala yaliohusu jamii kwa kuegemea mikabala ya kikoloni, kielimu, kimaisha, kifalsafa na ujenzi wa jamii mpya baada ya mkoloni kuondoka.

Nyimbo zinaweza kutumiwa katika kubainisha miktadha mbali mbali ya jamii. Kupitia miktadha hii, nyimbo zinaweza kutumiwa katika kujadili masuala ibuka katika jamii. Masuala ibuka ni mambo mbali mbali yanayotendeka katika jamii kwa wakati huo. Masuala ibuka yamekuwa yakibadilika kila uchao katika jamii. Masuala ya kijinsia ni mojawapo ya masuala ibuka ambayo yamekuwa yakibadilika kadri muda unavyobadilika. Masuala haya yamekuwa yakijihusisha na mbinu mbali mbali zinazotumika kufuatilia na kuelewa tofauti za kimaisha kati ya mwanamume na mwanamke na yanayojumuisha upatikanaji wa fursa na rasilimali pamoja na changamoto zinazowakabili. Ni masuala ambayo yamekuwa yakiathiri jamii kila mara kutokana na mabadiliko na utangamano wa jamii tofauti. Licha ya kwamba nyimbo za *twist* ziliimbwa katika miaka ya 1950-1980, nyimbo hizi zina mchango mkubwa katika kujadili masuala ya jinsia yanayodhihirika katika jamii kwa sasa.

Dhana za Uana na Jinsia katika Muktadha wa Kiafrika

Uana ni dhana ambayo iliasisiwa kule Uropa katika miaka ya 1970 na 1980 ili kuelekeza masuala ya kihistoria yaliyohusiana na jamii kwa kuchunguza masuala ya kike na kiume

kama yanavyotegemeana katika maisha ya binadamu kwa kuzingatia masuala ya kibayolojia (Bonnie, 2001). Masuala ya kiuana ndiyo yaliyosababisha kuchipuka kwa yale ya kijinsia ambayo yalinuia kuonyesha uhusiano katika majukumu ya kuwa mume au mke.

Dhana ya uana imejadiliwa na wataalam mbali mbali, baadhi yao ni kama vile; Kamusi Elezi ya Kiswahili (2016) ambayo inasema uana ni hali ya kuwa kike au kiume kimaumbile. Mwanakombo (2000) anasema kuwa, suala la uana ni kipengele muhimu ambacho kimepuuzwa katika tafiti za Kiswahili hasa ushairi wa Kiswahili. Anasisitiza kuwa, elimu kuhusu masuala ya kijinsia ni muhimu sana kwa sababu huchangia kuhamasisha umma kuhusu majukumu yao ya kazi, nafasi zao katika jamii na matarajio ya jamii kuwahusu. Hali hii huchangia kuimarisha ushirikiano mwema katika taasisi mbalimbali za jamii pamoja na kutambua na kuthamini mabadiliko ya kitamaduni yanayoendelea kutokea kila wakati. Tafiti ambazo zimefanywa katika nyanja nyinginezo zimeonyesha kuwa mwanamme amechukua nafasi ya kwanza ya kumtawala mwanamke (Mung'ahu, 2011). Kwa mfano, Ripoti ya UNICEF (1984) inaonyesha kuwa mwanamke amepewa nafasi ya mzazi na mlezi wa watoto, mtafutaji wa chakula na msimamizi wa shambani; nafasi ambayo ni ya hadhi ya chini katika jamii.

Kwa upande mwingine, jamii za Kiafrika humtukuza mwanamume kupitia mila, desturi na itikadi zao (Kobia na Mung'ahu, 2011). Momanyi (2007) anadokeza kuwa katika jamii ya Waswahili kuna itikadi zinazohalalisha mamlaka ya mwanamume kwa misingi ya desturi za kitamaduni, itikadi za kidini na tofauti za kijinsia. Katika muktadha huu mwanamume ana nafasi zifuatazo katika jamii: Kwanza, utawala wa mwanamume umehalalishwa katika kila sehemu ya maisha kwa kusisitiza maumbo ya vitambulishi vya jinsia ya kiume kwa misingi ya jamii, maandishi, matukio na maelezo ya kihistoria. Pili, wanaume wametawala na kuwa na mamlaka makuu katika jamii kwa kushikilia nafasi za rasilimali zenye thamani katika jamii kama vile kazi, pesa na taasisi za kijamii zenye nguvu kama vile serikali na dini. Tatu, desturi za jinsia ya kiume zimehalalishwa kwa madai kuwa wanaume husukumwa kutenda kulingana na ubabedume. Aidha, nguvu za mwanamume zinajidhihirisha kama nguvu za kimwili, shujaa, kufanya kazi na kukidhi familia, kuwa na tajriba, mkakamavu, razini, anayejitakia makuu, majivuno, mwadilifu na mshindani (Kobia na Mung'ahu, 2011). Kutokana na maelezo haya, masuala ya kijinsia yanahusu kitengo cha jamii ambacho kimetambuliwa na jamii kuimarisha tofauti za majukumu ya mwanamke na mwanamume.

Misingi ya Nadharia

Makala hii iliongozwa na na nadharia ya Ufeministi katika muktadha wa Kiafrika iliyoasisiwa na Steady (1981) na kuendelezwa na Nyangweso (2017). Nadharia hii inachunguza hali za kijamii na kitamaduni katika muktadha wa Kiafrika. Nadharia hii hudhamiria kuonyesha kwamba uana na uhusiano kati ya mwanamke na mwanamume ni mambo ya kati kabisa katika fasihi. Nadharia hii huchunguza hali za mwanamke katika jamii ambazo zingewekwa na harakati za ukombozi wa jamii mpya kwa kuwa ufeministi ni siasa ya ukombozi wa mwanamke katika jamii ambayo imejaa mivutano ya kijinsia, kisiasa, kiutamaduni na kiuchumi.

Baadhi ya mihimili muhimu ya nadharia iliyozingatiwa katika makala hii ni kama vile; fasihi kama jukwaa la kueleza kwa uyakinifu hali aliyomo mwanamke ili kumsaidia mtu yeyote kuelewa hali hiyo. Nyimbo za Daudi Kabaka na John Nzenze zinatuchorea taswira kamili ya mwanamke katika jamii. Senkoro(1982) anaeleza kuwa, waandishi na wahakiki wa fasihi za Kiafrika wanakumbana na wanawake waliojipamba, wanaonukia manukato makali, waliovaa nguo zinazolenga kuwavutia wanaume ili wawape pesa na kushirikiana nao kimwili. Katika muktadha huu mwanamke amepewa nafasi hafifu kabisa katika jamii ambayo haimhusishi katika uzalishaji wa mali.

Mhimili mwingine muhimu ni ule ambao unanuia kusawazisha wanadamu kwa upande wa utamaduni na uana. Licha ya kwamba nadharia ya ufeministi wa kiafrika ni nadharia inayokinzana na mikabala ya kiumeni inayoonekana kupendelea wanaume na kuwanyanyasa wanawake, nadharia hii pia hulenga pia kutatua matatizo yanayowakabili wanawake katika jamii inayotawaliwa na wanaume. Hivyo basi, ufeministi katika muktadha wa Kiafrika ni nadharia inayolenga kupigania haki za wanawake na kuweka wazi matatizo yanayowakumba pamoja na kutoa mapendekezo kuhusu namna ya kuyatatua. Nyimbo za Daudi kabaka na John Nzenze zinatuchorea hali halisi ambazo mwanamke amekuwa akizipitia kama vile, kuwa mlezi, dhuluma nyingi, na kiumbe duni aliyefinyangwa na minyororo ya utamaduni. Aidha nyimbo hizi zinatuchorea taswira kamili ya namna wanaume wanavyoendeleza harakati zao za ukandamizaji wa wanawake kwa mfano kupitia ulindaji wa mila na tamaduni za kijamii.

Aidha, makala hii ilizingatia mhimili unaotambua umoja wa wanawake katika ukombozi wao. Wanawake wana jukumu la kuhakikisha kwamba wanajikomboa kutoka kwa dhuluma zinazoendelezwa na wanaume. Ukombozi huu ungetokana na wao wenyewe kuwa mstari wa mbele kuhakikisha kwamba wanajikomboa kutokana na mila na tamaduni zinazowakandamiza. Nyimbo za Daudi Kabaka na John Nzenze zinampa mwanamke nafasi ya kujikomboa kwa mfano kupitia uwezo wake wa kupata elimu ambayo ingempevusha kimawazo na kuhakikisha kuwa anapigania usawa katika jamii. Hivyo basi nadharia hii ilikuwa muhimu katika kueleza mahusiano ya mwanamume na mwanamke katika jamii pamoja na changamoto zilizokumba maisha yao kimahusiano.

Mbinu za Kukusanya Data

Data muhimu za makala hii zilitoka kwa nyimbo zilizorekodiwa, kwa hivyo njia na mbinu za maktaba zilikuwa muhimu katika utafiti huu. Uchunguzi wa kimaktaba ulihusu uorodheshaji wa nyimbo na taarifa za kimsingi kutoka kwa wanamuziki hawa. Aidha, mkabala wa kiethnografia ulitumiwa katika kukusanya data za kimaelezo kuhusu tamaduni za jamii ambapo wanamuziki hawa walizaliwa ili kuchunguza kwa undani falsafa zinazojitokeza katika nyimbo zao. Uchunguzi wa kiethnografia ulizingatia maelezo ya kina ya watu katika mazingira yao kupitia mbinu za utafiti kama vile uchunzaji wa kushiriki na mahojiano ya ana kwa ana kwa nia ya kueleza utamaduni wa jamii katika njia iliyo wazi kabisa. Mtazamo wa kiethnografia ulisaidia katika kukusanya data kuhusu maoni ya watu kuhusiana na yale yaliopo, yale yanayokubalika, yale watu wanayafanya, wanasema na jinsi wanavyoshirikiana katika kufanya kazi (Dewan, 2018).

Kwa kuzingatia mkabala wa kiethnografia, makala hii ilichunguza nyimbo hizi kwa kuangazia wanamziki hawa katika mazingira yao kwa kuhoji wazee watano kutoka jamii yao. Uteuzi wa wazee hawa ulikuwa wa kimaksudi. Wazee hawa walikuwa watu ambao wameishi enzi za Daudi Kabaka na John Nzenze. Aidha John Nzenze alishiriki katika kutoa maelezo yake kuhusiana na usuli wa baadhi ya nyimbo walizoimba na mahusiano yake ya Daudi Kabaka. Ingawa nyimbo hizi ziliangazia mambo mbali mbali katika jamii, ni dhahiri kuwa nyimbo hizi pia zilijadili masuala ya jinsia yalioathiri jamii wakati huo.

Nyimbo za Daudi Kabaka na John Nzenze

Wanamuziki Daudi Kabaka na John Nzenze ni waimbaji wakongwe waliovuma sana katika miaka ya 1950, 1960 na 1970. Nyimbo zao zilifahamika kwa mtindo wa *twist*. Nyimbo za *twist* kwa sasa zinajulikana kama *zilizopendwa* kwa maana ya nyimbo zilizokuwa maarufu sana. Nyimbo za *twist* ziliiga mtindo maarufu wa nyimbo zilizopatikana katika Afrika Kusini za *kwela* katika miaka ya 1950. (*Kwela* ni jina la Zulu lenye maana kuwa mwangalifu). Mitindo ya *kwela* ilikuwa ikitumia zumari maalum ambayo ilikuwa kama ala kuu ya kuwahamasisha wakaazi wa vibandani hasa walipokuwa wakistarehe kwa mvinyo haramu

kuhusiana na kuwasili kwa maafisa wa polisi. Maafisa hawa wa polisi walikuwa wakiwawinda walevi haramu katika sehemu zao za burudani(Lara,1999).

Wanamuziki Daudi Kabaka na John Nzenze walitoka katika jamii ya Waluhya japo nyimbo zao ziliimbwa katika lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo nyimbo zao zinaweka msingi wa utanzu wa nyimbo *zilizopendwa* ambazo zimeendelea kuenziwa kwa miaka mingi. Jamii ya Waluhyia ni jamii ambayo ina utamaduni, mila na itikadi sawa na ni dhahiri kwamba mambo haya yaliathiri dhamira na maudhui katika nyimbo zao. Ni wanamuziki walioishi katika wakati wa ukoloni na baada ya uhuru na walishuhudia mabadiliko mengi yaliyokuwa yakitendeka katika jamii ya Waluhya.

Baadhi ya nyimbo ambazo waliimba zilikuwa na mtindo wa kipekee wa *twist*. Daudi Kabaka aliimba nyimbo kama '*African twist', Harambee Harambee Shauri Moyo, Shemeji Lumbe* na *Western Shilo* Pia aliimba wimbo wa *Helule Helule* ambao ulivuma sana katika mataifa ya Ulaya. '*Harambee Harambee*' ambao ni wimbo unaosisitiza umuhimu wa wananchi wa Kenya kujenga nchi yao baada ya kujinyakulia uhuru kutoka kwa mkoloni. 'Harambee' ni dhana iliyoanzishwa na Rais wa kwanza wa Jamhuri ya Kenya yaani Jomo Kenyatta. Dhana hii ilikuwa na maana ya kuvuta pamoja kwa wananchi wote ili washirikane katika uzalishaji wa mali na katika kupiga hatua za kimaendeleo.

Pia John Amutabi Nzenze, ni mwanamuziki wa Kenya kutoka jamii ya Waluhya. Baadhi ya nyimbo zake maarufu ni kama vile *Angelike, Julieta Rudi Tuonane Ninamliya Susana* na *Habari za Nairobi.* Baadhi ya nyimbo alizoimba na Daudi Kabaka ni kama vile *Masitsa, Bachelor Boy, Rehema, Safari ya Tanganyika, Taabu ya Mawnamue* na *Nyumba za Tobacco.* Ni mwanamuziki ambaye ana tajriba kubwa ya maisha hasa baada ya kutumbuiza mashabiki katika sehemu mbalimbali za ulimwengu. Amezuru nchi kama vile Ujapani, Algeria, Ethiopia, Ujerumani miongoni mwa mataifa mengine. Bendi yake ilifahamika kama *Air Fiesta Matata* ambayo ilitunukiwa tuzo na rais wa kwanza wa Jamhuri ya Kenya, Mzee Jomo Kenyatta.

Masuala ya Jinsia katika Nyimbo za Daudi Kabaka na John Nzenze

Nyimbo za Daudi kabaka na John Nzenze zina mawazo mengi yanayohusiana na masuala ya jinsia katika muktadha wa jamii yao. Masuala haya yanahusu miktadha ya kisiasa, kijamii, kiuchumi, kielimu na kiteknolojia. Mwanamke ana sifa za kiuana zifuatazo:

Kiumbe anayestahili kumpenda Mwamamume na kuishi kwa boma

Kupitia kwa wimbo wa *Safari ya Tanganyika* mwanammke anaonekana kama anayeachiwa wajibu wa kulinda boma. Mwanamume anaondoka kwenda safari ya Tanganyika kujitafutia riziki huku akimwacha mkewe akichunga boma. Kwa mfano msanii anasema:

Masitsa, mimi naenda Safari Tanganyika,
usilile machozi sana mimi nitakonda
Masitsa nitarudi mpaka tuonane

Aidha, msanii anamsihi mchumba wake kuwa hatakuja kuoa mchumba mwingine. Anasema kuwa hata ingawa anaondoka kwenda Tanganyika, mchumba wake atabakia kwenye moyo wake na kamwe hatamsahau.

Usidhani nitamuoa mwingine Tanganyika.
Hata mimi nikitembea nakuaza Masitsa
Nifanyaje safari yangu sasa itavunjika.

Hali kama hii inampa mchumba wake uwezo wa kustahimili maisha yake bila kuwa na mchumba wake.

Aidha kupitia wimbo wa '*Safari ya Tanganyika'*, mwanamume amapewa jukumu la kuamua mambo muhimu ya jamii. Kwa mfano,anaodoka kwenda kutafuta kazi ili aweze kukimu jamii yake. Licha ya kuondoka katika hali tatanishi ambayo haikuwa imekubaliwa na mkwewe, msanii ana imani kuwa atakapomaliza ziara ya Tanganyika, atarejea nyumbani na kuendele kukimu jamii.

Kupitia kwa wimbo wa *Rehema* msanii anasema kuwa, licha ya kwamba wametengana na Rehema, anasisitiza kuwa Rehema atakuja kukumbuka yale waliyoyafanya naye. Hali hii inamaanisha kuwa mwanamke ni kiumbe msahaulifu. Kupitia nyimbo hizi ni dhahiri kuwa mwanamke amesawiriwa kijinsia kama kiumbe anayestahili kumpenda mwanamume na kubakia kwa boma iwapo mwanamume ataondoka kwenda mjini kutafuta kazi au kutafuta namna ya kukimu familia yake na pia kiumbe atakayekumbuka uhusiano wake na mume wakitengan

Katika jamii nyingi za Kiafrika, mwanamume alishikilia nafasi ya kuwa kiongozi wa jamii. Alihitajika kuiongoza jamii kupitia uzalishaji mali, kuilinda kutokana na adui na kuipa mwelekeo. Hali hizi zinadhihirika katika nyimbo za hawa wanamuziki kama wimbo wa *Taabu ya Mwanamume* wanasisitiza kuwa mwanamume anahitaji kufanya kazi ili aweze kujikimu kimaisha. Matini ya wimbo huu yanayobeba haya maudhui ni:

Ukizaliwa wewe ni kijana, ukose kazi taabu yote itakupata x2
Ohoo ohoo Tali Malina baby, umeniacha ati sina kazi
Ukienda kuona mtu wa kwenu, ukitoka wanaanza masengenyo x2
Huyu kijana kazi gani anataka, kupeleka ndege ama kupeleka gari
Oh ohoo kazi ni ngumu mama, nimetafuta sasa nimeshindwa
Lakini bwana wewe ukumbuke, kazi ya mzungu lazima utafutwa

Mwanamume hana budi kuondoka katika boma lake ili akaende katika miji kwa minajili ya kujitafutia kazi ili kujikimu kwake yeye na jamii yake kimaisha

Mwanamke kama Mpenda Anasa na Maringo

Maudhui haya yanajijotokeza katika wimbo wa *Msichana wa Elimu*. Katika wimbo huu, msanii amemsawiri msichana kama aliyepata elimu ya juu hasa kutoka Ulaya. Japo msichana huyu ana elimu ya juu, hajaolewa. Katika muktadha wa Kiafrika, elimu ya mtoto msichana haikuwa muhimu sana. Kuendeleza kizazi kwa kuwazaa watoto ni jambo ambalo lilipewa msukumo mkubwa. Kwa mfano msanii anasema yafuatayo:

Msichana wa sura nzuri
Kitu gani kinakufanya usiolewe
Elimu unayo ya kutosha
Hata ng'ambo ukaenda ukarudi
Ooh baby
Ona watoto wa nyuma yako
Wameolewa wamekuacha ukihangaika

Kwa hivyo, msanii anahoji sababu ambazo zimefanya huyu msichana asiolewe. Msichana huyu hastahili kuwa na majivuno kwa vijana kwa sababu ni hawa vijana ambao watamwoa. Katika jamii za mfumodume swala la mwanamke kuolewa hususitizwa sana kuliko mwanamume kutooa Msichana hutarajiwa kuolewa ili aweze kuendeleza kizazi chake

na cha mumewe.Watoto katika muktadha wa Kiafrika walikuwa kama nguzo kuu ya familia kunawiri.

Mwanamke kama Mlezi na Mhimili Mkuu wa Ndoa

Kimsingi, asasi ya ndoa hujengwa na mwanamke katika jamii ya Kiafrika. Mama anatarajiwa kuwa mlezi mkuu katika jamii za kiafrika. Maudhui haya yanadhihirika kupitia wimbo wa *Pole Musa*. Katika wimbo huu, mwanamke amesawiriwa kama kiumbe mvumilivu katika ndoa. Licha ya vichapo na mateso ya kila mara kutoka kwa mumewe, ameendelea kuishi katika ndoa yake.

Musa nimevumilia sana, Musa nimevumilia sana
Kupigwa pigwa kama mimi punda, Na sura yangu imeharibika
Na ngumi zako za kila siku Musa,Taabu…..,Taabu….Taabu….
Kweli musa, Uliponioa,
Sura yangu, Haikuwa na alama
Hata moja…….
Nilikuwa na afya nzuri, Nilinona, kama ngoimaya kirige…..

Musa ambaye ni mhusika mkuu wa kiume katika wimbo huu amesawiriwa kama mtu ambaye ni katili sana kwa mwanamke wake. Mathalan, sura ya huyu mwanamke alipoolewa ilikuwa nzuri sana na haikuwa na alama hata moja. Sura ya huyu mwanamke imeendelea kunyauka kwa sababu ya mateso yake Musa. Katika muktadha huu, ni dhahiri kwamba mwanamke ni nguzo kuu katika ndoa. Mwanamume anastahili kumlinda na kumhifadhi mwanamke badala ya kuwa na mateso kwa mwanamke.

Aidha **s**uala la kulinda jamii ni jambo ambalo limetwikwa mwanamume. Ulinzi huu unahusu ukingaji wa jamii kutokana na vikwazo vya kiusalama, kiuchumi, kitabaka na kielimu. Kupitia kwa wimbo wa '*Kabaka Says'* mwanamume amempachika mwanamke asiyejiweza katika jamii mimba na amemtelekeza. Msanii anasisitiza kuwa unapozaa na mwanamke kwa mfano kiwete ni sharti uchukuwe mtoto. Mwanamume kwa hivyo amesawiriwa kama mlinzi mkuu wa jamii yake

Kuendelezwa kwa Kizazi cha jamii mara nyingi hutegemea mwanamume. Mwanamume ana jukumu la kuendeleza kizazi kupitia kuoa. Kupitia wimbo wa *Bachelor Boy* msanii anamwangazia mtoto mvulana ambaye ameshindwa kuoa kwa sababu ya kupenda raha nyingi. Wimbo huu unaendeleza maudhui haya katika mishororo ifuatayo;

Mimi ni bachelor boy, nitaoa kutoka wapi
Na siku sasa zimepita, looo sireraela
Sababu nikose kuoa, nikupenda raha nyingu
Bachelor boy wenzangu, Twist! Twist!
Wasichana hutuma barua, niende kwetu niwaoe
Lakini mimi siwezi kuacha raha za mjini

Hivyo basi, mwanamume anahitaji kutojiingiza katika raha nyingi ili kuoa mke kwa minajili ya kuendleza kizazi. Anatarajiwa kuoa mwanamke ili kuendeleza kizazi chake.

Mwanamke kama Mzinzi

Uzinzi katika ndoa za kiafrika ulichukuliwa kama kosa kubwa sana kwa mwanamke. Masuala haya yanadhihirika katika wimbo wa, *Shauri Moyo*. Msanii anasema kuwa alikuta mkewe wa kwanza Nairobi wakapendana, hadi akaenda naye kwa nyumba yake Shauri Moyo

Alipokuwa amelala alisikia ‘fungua mlango mimi ni mwenye nyumba’. Kwa mfano msanii anasema:

Nikuta bibi wa kwanza Nairobi
Akanipenda name nikampenda
Nikamuuliza kama ana bwana
Akanijibu sina hata mpenzi
Tukaenda naye mpaka kwake
Shauri moyo kwa nyumba za Tumbaku
Nilipolala kasikia hodi hodi
Fungueni mini ni mwenye nyumba….

Kupitia wimbo huu ni dhahiri kwamba uzinzi katika ndoa ni jambo ambalo halikuwa linakubalika hasa ikiwa ungetekelezwa na mwanamke. Mwanamke alitarajiwa kuwa mwaminifu katika ndoa ili kuepukana mizozo ya kindoa

Hitimisho

Kutokana na mjadala huu ni dhahiri kwamba, nyimbo za Daudi Kabaka na John Nzenze zina maudhui na dhamira nyingi za masuala ya kijinsia yanayohusishwa na wanaume na wanawake. Masuala haya huangazia wema na upungufu wa kila mwanajamii. Kwa mfano, mwanamume amesawiriwa kama; nguzo ya jamii katika hali zote, mwendelezaji wa kizazi chake, mwamuzi na mlinzi mkuu. Vile vile, mwanamke amesawiriwa kama; mpenda mwanamume na anayefaa kukaa katika boma, chombo cha kustarehesha mwanamume na kuendeleza kizazi, mlezi na mhimili mkuu katika ndoa na mjenzi wa jamii yake.

Mabadiliko katika masuala ya kijinsia yamekuwa yakishuhudiwa katika jamii. Usawiri wa wanawake katika jamii umeendelea kuwa na msukumo wa usawazishaji wa majukumu bila kuangazia tofauti za kiuana. Kutokana na hali hii, wanaume wameweza kushuhudia ushindani mkubwa kutoka kwa wanawake. Jambo ambalo linabadilisha mkondo wa mawazo finyu kuwa, wanawake ni viumbe dhaifu. Licha ya kuamba nyimbo za Daudi Kabaka na John Nzenze ziliimbwa katika miaka ya 1950 hadi 1980 masuala ya kijinsia yaliozingatiwa katika nyimbo hizi yangali na umuhimu mkubwa katika jamii ya sasa. Japo pamekuwepo mabadiliko katika wakati, maudhui katika nyimbo hizi yanasawiri mwanamke na mwanamume katika uhalisia wa maisha ya jamii.

Marejeleo

Bonnie, G. S. (2001) *Gender Theory.* In encyclopedia of European social history. The Gale Group Inc.

Chiduo F. K. E na Wenzake (2016) *Kamusi elezi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

King’ei, K. na Kisovi, M. N. C. (2005) *Msingi wa fasihi simulizi.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Dewan, L. (2018) Understanding ethnography: An exotic ethnographer’s perspective. In P. Mura, C. Khoo-Lattimore (Eds). *Asian qualitative research in tourism; Perspective on Asian tourism*. Singapore: Springer.

Kobia, J. M. na Mung’ahu, R. (2011) ‘Ubabedume katika ushairi wa Kiswahili: Mfano wa utenzi wa Fumo Liyongo’ katika *Kioo cha lugha Juzuu 11*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University.

Lara, A. (1999) Kwela: The structure and sound of Pennywhistle. Music-ISBN-1-85928-143-5.

M’Ngaruthi, K. T. (2008) *Fasihi simulizi na utamaduni*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Mulokozi, M. M. (1989) ‘Tanzu za Fasihi Simulizi’ katika *Mulika*, Jarida la TUKI Na. 21.

Mung'ahu, R. S. (2011) *Usawiri wa Mwanamume katika Ushairi wa Kiswahili. Mfano wa Utenzi wa Fumo Liyongo na utenzi wa mwanakupona*. Tasnifu ya M.Ed Kiswahili, (Isiyochapishwa), MMUST, Kakamega, Kenya.

Mwanakombo, N. (2000) Tools of gender analysis in Kiswahili research. Katika *Utafiti wa Kiswahili.* Moi University Press.

Nyangweso, M. S. (2017) *Nafasi na athari ya kiongozi wa kike katika tamthilia teule za Kiswahili.* Tasnifu ya M. A. (Isiyochapishwa), Masai Mara University, Narok, Kenya.

Senkoro, F. E. M. K (1982) *The prostitute in African literature.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Simala, I. (2006) 'Fasihi simulizi katika enzi ya utandawazi' katika *Fasihi Simulizi ya Kiswahili.* Nairobi: Twaweza Communications na CHAKITA Kenya.

Steady, C. F. (1981) *The black woman cross culturally*. Schenkman.

TUKI (2010) *Kamusi ya Kiswahili sanifu.* Dar es Salaam: TUKI.

UNICEF(1984) 'Situation analysis of children and women in Kenya'. *The Roles and Situation of Women*. Nairobi: Central Bureau of Statistics.

Wafula, R. na Njogu, K. (2007) *Nadharia ya uhakiki wa fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation Publishers.